ponitembelea, nilikuwa nasubiri kwenda kustarehe na bwana KUPEPESA. Niliwakaribisha kwa shingo upande, ila sikuwa na hamu ya kuwasikiliza. Kula bata na bwana Kupepesa, ndilo jambo pekee lililokuwa moyoni mwangu.

Kupepesa ni jina la utani alilopewa, kutokana na macho yake kutokuwa na pazia pale mabinti walipopita mbele zake. Masuala ya baba huyu ni mengi, ila kwa kuwa hayamletei Mungu utukufu, niseme tu kuwa siku hiyo niliamua kujiunga na UKRISTO WA KWELI. Kupepesa alipokuja, alinikuta nikifurahia maisha mapya ndani ya Kristo. Huo ukawa mwisho wa mahusiano kati yangu naye!

Katika kuagana na dada Sijali, nilimwuliza ikiwa huko kuzimu wako viongozi, wanaofahamika huku duniani kama viongozi wa kiroho. Viongozi hawa ni pamoja na Makadinali, Mitume, Manabii, Maaskofu, Wachungaji, Wainjilisti, Wazee wa kanisa, Mashemasi, Mashehe, Maimamu na kadhalika. “Wamejaa tele,” alisema dada Sijali! “Hata hivyo kutokana na kazi nzuri waliyomfanyia Shetani ya kuwapotosha wafuasi wao, wametengewa mtaa wao unaojulikana kama mtaa wa na DUA na MAPAMBIO. Umepewa jina hili, kutokana na dua wanazozifanya mara kwa mara zilizochanganyika na nyimbo za kidini, kama ishara ya kutubia maovu yao!”

Karibu niangue kicheko, pale aliponieleza kisa cha kiongozi aliyekaribia kupigwa na waliokuwa wafuasi wake, kwa madai kuwa alipenda pesa zao kuliko roho zao! Hata hivyo ugomvi huu uliamuliwa na mmoja wa walinzi wa kuzimu, anayefahamika kwa jina la MAJUTO NI MJUKUU! Sijali aliendelea kunifahamisha kuwa alipofika kuzimu, alishangaa pale alipomwona mwanzilishi wa moja ya dini zenye wafuasi wengi duniani. Alitaja kutoamini Uungu wa Yesu na uwezo wa damu yake katika kuokoa, kama sababu kuu iliyompeleka kuzimu. Kutokana na kazi aliyoifanya ya kupoteza wafuasi wake, amepewa jukumu la kupokea wafuasi wake wanaofika kuzimu!

Katikati ya maongezi yetu, dada Sijali alilia kwa uchungu, mithili ya mtu aliyechomwa na kisu moyoni. Hapo nilitambua kuwa alikuwa anaelekea kuzimia. Wakati kilio hiki kikiendelea, nilizinduka huku nikitetemeka. Siku iliyofuata nilianza kwenda maofisini, viwandani, magerezani, mashuleni, hospitalini, majumbani, vijiweni na kwenye hosteli za wana vyuo, kusimulia maono haya na jinsi Mungu alivyomtuma Yesu Kristo duniani, ili kuzuia watu wasiende kuzimu (Yohana 3:16). Yule aliyekataa kuamua kuwa Mkristo wa kweli, nilimhurumia na kuendelea kumwombea.

Kwa wale walioamua kukubaliana na ujumbe wangu, niliwasihi waombe sala ifuatayo kwa kumaanisha. “Mungu Baba, nimegundua kuwa mimi ni mwenye dhambi na sitaki kuendelea kuishi dhambini. Naomba unisamehe dhambi zangu na kunifanya kuwa mtoto wako. Ninampokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wa maisha yangu, na ninaahidi kuishi maisha yanayokubaliana na neno lako. Ninaamini kuwa umenisamehe na leo hii nimeokoka. Amen.”

## WASILIANA NASI

Baada ya kuomba maombi haya, wasiliana nasi ili tufurahi pamoja nawe na kukuelekeza katika kanisa litakalokufundisha jinsi ya kushinda dhambi, magonjwa na kazi zote za Shetani.
Ni mimi **ASKOFU RODRICK MBWAMBO,** mwandishi wa kipeperushi hiki. Shalom!


## MARANATHA RECONCILIATION CHURCH

**S.L.P 7812 Dar es Salaam, Tanzania**
**SIMU: +255 766 109 285 KWA DAR ES SALAAM**
**SIMU: +255 689 998 039 KWA DODOMA .**
**Barua pepe: maranathayahwe@gmail.com**


# Simu YENYE UTATA



MUDA mfupi ulikuwa umepita, tangia tumzike mfanyakazi mwenzetu dada Petepete. Petepete ni jina la utani, alilopewa kutokana na wingi wa pete za dhahabu vidoleni mwake. Ingawa mshahara wake ulikuwa mdogo kama wangu, pete hizo zilitokana na kujiuza kwa wanaume. Kama vilivyo vifo vya watu wa tabia kama yake, kifo chake kilikuwa kinatarajiwa. Miezi michache kabla ya kuaga dunia, maneno yalisikika mitaani kuwa anaugua ugonjwa wa kisasa! Nifupishe kwa kusema kuwa tulimzika katika makaburi yaliyoko mtaa wa SIKUOKOKA, wanamwozikwa watu waliokataa kuwa Wakristo wa kweli.

Nikijua aina ya maisha aliyoyaishi, nilisononeka mno wakati wa kuaga mwili wake. Niliutazama kwa huzuni na kusema, "hakika mshahara wa dhambi ni mauti!" (Warumi 6:23). Baada ya kuzika, nilijilaza mchagoni huku nikifikiria kule roho yake ilipo. Katikati ya huzuni hii, fahamu zilinitoka mithili ya mtu aliyedungwa sindano ya ganzi. Hapo nilisikia mlio ukiita, mithili ya mlio wa simu. Mlio huu ulipokatika, nilisikia sauti iliyochanganyika na kilio ikiita jina langu.

Ilikuwa ni sauti ya dada Sijali, aliyeaga dunia miaka sita iliyopita. Kama ilivyokuwa kwa Petepete, alipewa jina hili, kutokana na kutojali Habari Njema za Wokovu. Kila alipoelezwa kuhusu UWEZO wa DAMU ya Yesu katika kuokoa, aliishia kutikisa kichwa, kama ishara ya KUTOJALI! Katika kile kilichoonekana kama kukwepa kuwaongezea wafiwa maumivu, sababu ya kifo chake, haikuelezwa wakati wa mazishi. Hata hivyo tuliokuwa karibu naye, tulijua kuwa alifariki katika harakati za kutoa mimba.

Kwa kuwa mwili wake ulikuwa kisima cha watu wengi, kulikuwa na utata kuhusu mtu aliyempa uja uzito. Baada ya panga pangua ya hapa na pale, zigo lilimwangukia kijana anayeishi mtaa wa UTAJUTA! Baada ya kukosa nafasi katika makaburi ya WATAKATIFU, tulimzika dada Sijali katika makaburi yaliyoko mtaa wa SIKUOKOKA.

Sijali alipiga simu, kunijulisha kuhusu kuwasili kwa dada Petepete huko kuzimu. Akiongea kwa sauti yenye mikwaruzo, alinieleza kuwa aliwasili huko mara tu alipokata roho, katika hospitali ya UTAKOMA UBISHI. Alinieleza kuwa alipofika kuzimu, alishangaa kuona watu wote wakiwa weusi kama mkaa. Katika kuduwaa huku, alifahamishwa kuwa naye atakuwa hivyo muda mfupi ujao!

Akiwa katika hali hii ya kushangaa wenzake, funza alimng'ata shingoni na kutokea upande wa pili. Maumivu ya shambulizi hili yalisababisha apige yowe, mithili ya mtu aliyekanyaga makaa ya moto. Hata hivyo, hakuna aliyeonekana kujali au kumhurumia! Hapo nikakumbuka maneno aliyosema Bwana, kuwa huko funza wake hawafi wala moto wake hauzimiki, tena kuna kulia na kusaga meno! (MT 13:42).

Nikiwa katika hali ya kushangaa maono haya, nilitaka kujua matokeo ya misa ya wafu aliyofanyiwa dada Petepete, katika dhehebu la WASIOJUA Maandiko. Wakati nikisubiri jibu, nilisikia kilio kikubwa mithili ya mtu aliyedungwa msumari wa moto. Baadaye, Sijali alinieleza kuwa kilikuwa kilio cha Petepete, baada ya kuangukiwa na libaba lililozidiwa na ukali wa moto!

Ili kuniweka sawa, alinifahamisha kuwa mwanamume huyo ni yule aliyekuwa akibadilisha wanawake, katika mitaa ya KIBURI CHA PESA na TAMAA YA MACHO. Jina lake lilikuwa halifahamiki, ila watu walizoea kumwita ZIPU MKONONI, kutokana na kutawaliwa na pepo la zinaa. Mbali na zinaa alikuwa mlevi wa pombe, huku akiihalalisha kwa kusema "hata Yesu alitengeneza pombe!"

Baba huyu alikufa ghafla, kiasi kilichomfanya akose nafasi ya kutubu. Kwa kuwa nilikuwa nikimweleza habari za wokovu mara kwa mara, nilishiriki kumzika katika makaburi ya WAPINDISHAO maandiko.

Kuwasili kwa dada Petepete huko kuzimu, kunapingana na mafundisho ya uongo ya mahali paitwapo 'pugatori,' na msamaha unaotokana na misa za wafu. Haya ni mafundisho tu yanayotumiwa na Shetani, kuongeza idadi ya waendao kuzimu. Biblia haioneshi kuwa kuna ahueni yoyote, pale mtu asiye Mkristo wa kweli anapokufa. Badala yake inasema, "mwanadamu amewekewa kufa mara moja na baada ya kifo ni hukumu" (Waebrania 9:27).

Niliendelea kuongea na dada Sijali kwa taabu, kutokana na sauti yake kuingiliwa mara kwa mara na vilio na maombolezo! Nilipomwuliza kuhusu watu walioko kuzimu, alianza kwa kunielezea maana ya kuzimu. Alinifahamisha kuwa kuzimu ni maskani ya muda, ya roho za watu waliokataa kuwa Wakristo wa kweli. Nilishangazwa na uelewa wake, pale aliponifahamisha kuwa baada ya ufufuo wa mwisho, ndipo watu hawa watakapotupwa katika ziwa la moto (Uf 20:13-15).

Kuhusu watu walioko kuzimu, aliniambia kuwa ni pamoja na wale walioshika dini badala ya Ukristo wa kweli. Hawa wanapatikana katika ulimwengu wa uzinzi, ulawiti, usagaji, uchawi, kuabudu sanamu, utumiaji wa mihadarati, uangaliaji wa picha za ngono, wizi, ujambazi, ndoa za jinsia moja na utafutaji wa mali kwa njia zisizompendeza Mungu (Wagalatia 5:19-21).

Akionekana kujutia hali yake ya kukataa KUOKOKA wakati wa uhai wake, Sijali alinieleza kuwa alipofika kuzimu ndipo alipogundua UZURI wa kuwa Mkristo wa kweli. "Sasa natambua kuwa Yesu peke yake ndiye NJIA, KWELI na UZIMA," alisema huku akilia kwa uchungu (Yohana 14:6).

Aliendelea kunifahamisha kuwa katika miaka ya hivi karibuni, idadi ya vijana wanaofika kuzimu imeongezeka, kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Kwa kuwa alikuwa haelewi mazingira ya duniani ya sasa, alionekana kutojua sababu zinazochangia ongezeko hili. Hata hivyo mimi nilielewa kuwa utandawazi, ndio sababu kuu iliyo nyuma ya wingi wa vijana wanaokufa na kuingia kuzimu. Utandawazi huu umeongeza matendo ya giza, yanayokula miaka ya kuishi ya vijana.

Matendo haya ni pamoja na zinaa, madawa ya kulevya, utoaji mimba, ujambazi, ugaidi, uangaliaji wa picha za ngono, filamu na tamthilia zinazochochea tamaa za mwili, kutoonyeka, kutoheshimu wazazi, miziki ya kidunia, mahubiri yasiyokemea dhambi, mazingaombwe makanisani, kuabudu mafanikio ya kimwili, ndoa za jinsia moja, ubadilishaji wa jinsia, kutanguliza dunia badala ya msalaba wa Kristo na mambo mengine mafu yanayofanana na haya.

Katika kuongea na Sijali nilihisi ukali wa maumivu yake, kutokana na kuugulia mara kwa mara. Kuugulia huku, kulinikumbusha watu walionitaabikia hata nikaokoka. Siku wali-